



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SHERIA YA MTOTO
[SURA YA 13]

TAFSIRI YA KANUNI ZA MALEZI YA KAMBO ZA MWAKA 2012

Toleo hili la Sheria ya Malezi ya Kambo za mwaka 2012, Tangazo la Serikali Na. 153 la tarehe 04 Mei, Mwaka 2012, ni Tafsiri Rasmi iliyosanifiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kuchapishwa kwa mujibu wa kifungu cha 84 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Mbalimbali, Sura ya 1.

Dar es Salaam
28 April, 2016

GEORGE M. MASAJU,
Mwanasheria Mkuu wa Serikali

TANGAZO LA SERIKALI NA. 165 la tarehe 13/05/2016

SHERIA YA MTOTO
(SURA YA 13)

KANUNI

KANUNI ZA MALEZI YA KAMBO

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 157(b))

MPANGILIO WA VIFUNGU

1. Jina.
2. Tafsiri.
3. Matumizi ya Kanuni hizi.
4. Maombi ya kumlea mtoto wa kambo.
5. Watu wenye sifa za kuwa wazazi wa kambo.
6. Tathmini ya wazazi wa kambo.
7. Rejesta ya walezi wa kambo na watoto wa kambo.
8. Masharti ya malezi ya kambo.
9. Taarifa ya uchunguzi wa kijamii.
10. Uzingatiaji wa dini.
11. Majukumu ya walezi wa kambo.
12. Haki za walezi wa kambo.
13. Haki za watoto wa kambo.
14. Taratibu za kuwezesha walezi wa kambo na watoto wa kambo.
15. Taratibu za matibabu.
16. Ziara za ukaguzi katika malezi ya kambo.
17. Mpango wa malezi ya kambo.
18. Kusitisha kwa malezi ya kambo.
19. Kifo
20. Makosa

SHERIA YA MTOTO
(SURA YA 13)

KANUNI

KANUNI ZA MALEZI YA KAMBO

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 157(b))

Jina
T.s. Na. 153 la
2012

1. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Malezi ya Kambo za mwaka, 2012.

Tafsiri

Sura ya 13

2. Katika Kanuni hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-
“Sheria” maana yake ni Sheria ya Mtoto;
“mwombaji” ina maana ya mtu au watu endapo ni maombi ya pamoja anayeomba kuwa mlezi wa kambo;
“makao yaliyothibitishwa” ina jumuisha makao ya watoto yaliyoanzishwa kwa mujibu wa kanuni zilizotungwa chini ya Sheria;
“afisa mwidhiniwa” maana yake ni Kamishna wa Ustawi wa Jamii au mtu mwingine aliyekasimiwa mamlaka na Kamishna;
“mtoto” maana yake ni mtu aliye na umri chini ya miaka kumi na nane ambaye kuhusiana naye amri ya malezi ya kambo inatafutwa au imekwishatolewa;
“Kamishna” maana yake ni Kamishna wa Ustawi wa Jamii;
“Idara” ina maana ya Idara ya Ustawi wa Jamii;
“mtoto wa kambo” maana yake ni mtoto aliye chini ya uangalizi wa mzazi wa kambo au familia ya kambo;
“familia ya kambo” ina maana ya familia ambayo inamlea mtoto wa kambo chini ya Kanuni hizi;
“mzazi wa kambo” maana yake ni mtu, au watu kama ni maombi ya pamoja, ambaye mtoto amewekwa chini ya uangalizi wake kwa mujibu wa Kanuni hizi; na

Matumizi ya Kanuni hizi	“Afisa Ustawi wa Jamii” maana yake ni Afisa Ustawi wa Jamii wa wilaya, mji, manispaa au jiji. 3. Kanuni hizi zitatumika kwa malezi ya mtoto anayeolewa na mzazi wa kambo.
Maombi ya kumlea mtoto wa kambo	4.-(1) Mtu yeyote anayekusudia kulea mtoto wa kambo, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 32(2) cha Sheria, atawajibika kupeleka maombi kwa Kamishna kwa kutumia fomu Na.1 iliyoonyeshwa kwenye Jedwali. (2) Maombi chini ya kifungu kidogo cha (1) yanaweza kufanywa kwa pamoja. (3) Meneja wa makao yaliyothibitishwa au taasisi anaweza kupendekezwa kwa afisa wa ustawi wa jamii au Kamishna, kwamba mtoto alelewe na wazazi wa kambo ambao wameorodheshwa kwenye Rejista chini ya Kanuni hizi.
Watu wenye sifa za kuwa wazazi wa kambo	5.-(1) Watu wafuatao wanaweza kuomba kuwa wazazi wa kambo- (a) mume na mke ambao ni raia wa Tanzania, na endapo mume ana mke zaidi ya mmoja, jina la mke ambaye atakuwa mama wa kambo linapaswa kuonyeshwa kwenye maombi; (b) mtu ambaye hajaoa au kuolewa ambaye ni raia wa Tanzania; (c) raia wa kigeni mume na mke, na katika mazingira haya mmojawapo wa waombaji anapaswa kuwa ameishi Tanzania kwa muda angalau wa miaka miwili na nusu mfululizo kabla ya kuwasilisha maombi; na (d) raia wa kigeni ambaye ameishi Tanzania kwa muda usiopungua miaka miwili na nusu mfululizo kabla ya kuwasilisha maombi. (2) Mtu aliye na umri wa chini ya miaka ishirini na moja ataruhusiwa kuwa mzazi wa kambo. (3) Mtu anayeonekana dhahiri kuwa na umri wa miaka sitini na tano anaruhusiwa kuwa mzazi wa kambo. (4) Pale ambapo mtu aliye na umri wa miaka sitini na tano na zaidi ataruhusiwa kuwa mzazi wa kambo kulingana na hali ilivyo, mtoto wa kambo hataondolewa chini ya malezi yake isipokuwa kwa sababu zilizoainishwa chini ya kanuni ya 18.

(5) Mtu hataruhusiwa kulea watoto wa kambo zaidi ya watatu kwa wakati mmoja bila ya kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Kamishna.

Tathmini ya
wazazi wa
kambo

6.-(1) Kamishna, ndani ya siku saba baada ya kupokea maombi ya malezi ya kambo, atamwelekeza Afisa Ustawi wa Jamii anayehusika kufanya tathmini ya mwombaji au waombaji.

(2) Afisa Ustawi wa Jamii atafanya tathmini kwa kina juu ya kila mtu anayeomba kuwa mzazi wa kambo ili kuweza kubaini kama mtu huyo anaweza kutoa malezi yanayofaa kwa mtoto.

(3) Tathmini itakayofanyika chini ya kanuni ndogo ya (2) itahusu-

(a) kutembelea nyumba ya mwombaji au waombaji ili kuchunguza kama mazingira ya nyumbani yanaridhisha;

(b) kukutana na mwombaji au waombaji kuchunguza kama wanaweza kukidhi masharti ya malezi ya kambo, na ikiwa ni maombi ya malezi ya kambo kwa mtoto mahususi, kama mwombaji au waombaji wanaweza kukidhi masharti hayo mahususi kwa mtoto huyo;

(c) kupata uhakika kutoka kwa mtoto yeyote anayeishi na mwombaji au waombaji kuwa ameridhia malezi ya kambo yatolewe;

(d) kupata uthibitisho kutoka kwa mtu ambaye ni kiongozi wa hospitali ya Serikali au afisa wa afya aliyethibitishwa katika eneo husika kuwa mwombaji au waombaji katika makazi yao hakuna mtu mwenye maradhi ya akili ambaye anaweza kumdhuru mtoto; na

(e) kupata uthibitisho kutoka kwa afisa wa polisi wa kituo cha polisi kilicho karibu na mwombaji au waombaji kwamba hakuna mtu katika makazi yao ambaye ameshawahi kuhukumiwa kwa makosa yanayohusu unyonyaji wa mtoto, kumdhalilisha mtoto kingono na makosa mengine yanayoweza kumfanya mtu huyo asifae kuwa karibu na mtoto.

(4) Afisa Ustawi wa Jamii, ili kuweza kufanya maamuzi ya kufaa kuhusu ombi au maombi ya malezi ya kambo, atamtaka mhusika kuwasilisha-

- (a) udhamini wa maandishi kuhusiana na tabia njema ya mwombaji kutoka kwa wadhamini watatu wanaomfahamu mwombaji kwa angalau kipindi cha miaka mitatu ambapo kwa upande mwingine wadhamini wengine watakuwa ni majirani wa karibu na Afisa Mtendaji wa Kata, Afisa Mtendaji wa Kijiji au Afisa Mtendaji wa Mtaa kadri itakavyokuwa, na kwa upande wa maombi ya pamoja, Afisa Ustawi wa Jamii anaweza kuomba nyongeza ya udhamini; na
 - (b) endapo ataona inafaa, udhamini wa maandishi kutoka kwa mwajiri kuhusu tabia njema ya mwombaji au waombaji, ikiwa mwombaji au waombaji wameajiriwa.
- (5) Afisa Ustawi wa Jamii anapaswa kukamilisha na kuwasilisha taarifa ya tathimini ya mwombaji wa malezi ya kambo katika fomu Na.2 iliyoainishwa kwenye Jedwali, pamoja na viambatisho vyake, kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii ndani ya siku sitini tangu alipopokea maombi.
- (6) Taarifa iliyowasilishwa chini ya kanuni ndogo ya (5) pamoja na taarifa nyingine, itajumuisha-
- (a) taarifa zinazohitajika chini ya kanuni ndogo ya (2) na (3) za kanuni hii;
 - (b) maelezo kuhusu jina, umri, dini na kazi ya mwombaji au waombaji; na
 - (c) idadi na umri wa watu wengine wanaoishi kwenye makazi ya mwombaji au waombaji.
- (7) Afisa Ustawi wa Jamii, endapo anashughulikia ombi la kumlea mtoto au watoto mahsusi, atawasilisha kwa Kamishna taarifa ya uchunguzi wa kijamii kama ilivyoainishwa chini ya kanuni ya 9 pamoja na tathimini hiyo.
- (8) Kamishna atatathmini maombi, na kuyapatia uzito unaostahili taarifa ya tathimini iliyowasilishwa na afisa wa ustawi wa jamii, na atamjulisha afisa ustawi wa jamii na mwombaji au waombaji kuhusu uamuzi wa kukubali au kukataa maombi ndani ya siku tisini kutoka tarehe ya kupokea maombi hayo.
- (9) Kamishna, endapo maombi yamekubaliwa, atamsajili mwombaji au waombaji kama walezi wa kambo kwa mujibu wa kanuni ya 7.

(10) Kamishna wa Ustawi wa Jamii atahakikisha kwamba rejesta ya walezi wa kambo waliokubaliwa inawekwa kulingana na Fomu Na.3 iliyoainishwa kwenye Jedwali na itahifadhiwa katika ngazi ya kitaifa.

Rejesta ya
walezi wa
kambo na
watoto wa
kambo

7.-(1) Kila mlezi wa kambo anapaswa kupewa namba ya pekee au endapo ni maombi ya pamoja, namba ya pekee itatolewa kwa wanandoa, ambayo itatumika katika rejesta katika ngazi ya kitaifa na wilaya na katika nyaraka zote zinazohusu malezi ya kambo.

(2) Afisa wa Ustawi wa Jamii atahakikisha kwamba rejesta mpya ya walezi wa kambo ya wilaya iliyo na taarifa zote kulingana na Fomu Na.3 iliyoainishwa kwenye Jedwali inawekwa katika ngazi ya wilaya na nakala yake inawasilishwa kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii kila mwezi.

(3) Daftari ya walezi wa kambo iliyoainishwa chini ya kanuni ndogo ya (1) inaweza kutumiwa na Kamishna kumweka mtoto yeyote kwenye malezi ya kambo kwa ajili ya uangalizi wa muda mfupi kama ilivyoainishwa chini ya kifungu cha 53(7) cha Sheria au kwa ajili ya uangalizi wa muda mrefu kama ilivyoainishwa chini ya kifungu cha 32(4) cha Sheria.

(4) Mara mlezi wa kambo anapokubaliwa na kuingizwa kwenye rejesta ya wazazi wa kambo katika wilaya, manispaa, mji au ngazi ya halmashauri, Afisa Ustawi wa Jamii atawasiliana na makao yaliyothibitishwa kuangalia uwezekano wa kupata watoto wanaofaa kupewa malezi ya kambo.

(5) Mtu yeyote ambaye amesajiliwa kama mlezi wa kambo anapaswa kumjulisha Afisa Ustawi wa Jamii kwamba hahitaji tena kulea mtoto wa kambo na suala hilo litawekwa kumbukumbu kwenye rejesta.

(6) Kamishna wa Ustawi wa Jamii atahakikisha kwamba rejesta ya malezi ya kambo ambayo ni lazima iwe kwenye fomu inayofanana na Fomu Na.4 inahifadhiwa kwenye ngazi ya kitaifa na wilaya.

(7) Kila malezi ya kambo yatapewa namba ya pekee ambayo itatumika katika rejesta ya kitaifa na wilaya na katika nyaraka zote zinazohusu malezi ya kambo.

(8) Afisa wa Ustawi wa Jamii atahakikisha kwamba rejesta mpya ya malezi ya kambo ya wilaya kulingana na Fomu Na.4 iliyoainishwa kwenye Jedwali inawekwa katika ngazi ya wilaya na nakala yake inawasilishwa kwa Kamishna wa Ustawi

wa Jamii kila mwezi.

(9) Endapo mtoto wa kambo ataondolewa kutoka kwa mzazi wa kambo kwa mujibu wa kanuni ya 18(1)(a), rejista ya walezi wa kambo na rejista ya malezi ya kambo zilizopo katika ngazi ya wilaya na Taifa zitahuishwa upya kuonyesha kwamba mzazi huyo wa kambo hajaidhinishwa tena kulea watoto na sababu za mabadiliko hayo zitatolewa.

Masharti ya
malezi ya
kambo

8.-(1) Mtoto anaweza kuwekwa kwenye malezi ya mzazi wa kambo endapo mtoto huyo-

- (a) amewekwa chini ya amri ya uangalizi au amri ya mpito ya uangalizi, chini ya kifungu cha 18(1) cha Sheria;
- (b) amewekwa kwenye makao yaliyothibitishwa au katika taasisi chini ya amri ya malezi au amri ya usimamizi chini ya kifungu cha 32(1)(a) au kifungu cha 53(1)(c) cha Sheria;
- (c) amewekwa kwenye makao yaliyothibitishwa au katika taasisi na mtu yeyote chini ya kifungu cha 53(1)(c);
- (d) amependekezwa na Afisa Ustawi wa Jamii kuwekwa katika makao yaliyothibitishwa au taasisi kama sehemu ya usalama zaidi kwake chini ya kifungu cha 53 (1) (c);
- (e) anahitaji uangalizi wa muda chini ya malezi ya kambo kwa mujibu wa kifungu cha 53 (7) cha Sheria.

(2) Mtoto hatawekwa chini ya mzazi wa kambo isipokuwa kama-

- (a) mzazi wa kambo au wazazi wa kambo wamesajiliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya 6 (7);
- (b) ripoti ya uchunguzi wa kijamii imekamiliwa kwa mujibu wa kanuni ya 9 na Afisa Ustawi wa Jamii amethibitisha kwamba mzazi wa kambo anafaa kumlea mtoto huyo;
- (c) mzazi wa kambo au wazazi wa kambo wamekubali kumlea mtoto wa kambo kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa chini ya kanuni ya 11;
- (d) maslahi ya mtoto kwa kadri inavyowezekana yatatimizwa kuhusiana na malezi ya kambo na yamepewa uzito unaostahili katika kufanya maamuzi kulingana na umri wa mtoto.

(3) Ridhaa ya mzazi, wazazi au mlezi inahitajika kwa malezi ya kambo na inapaswa kutolewa kwa kuzingatia utaratibu ulioainishwa kwenye fomu Na. 6 iliyopo kwenye Jedwali na Afisa Ustawi wa Jamii atahakikisha kwamba mzazi, wazazi au mlezi wanaeleweshwa vizuri nia na athari za kisheria za malezi ya kambo.

(4) Endapo ridhaa ya mzazi au walezi haikupatikana, Kamishna anaweza kuachana na masharti ya kupata ridhaa ya wazazi kama amejiridhisha kwamba-

- (a) mtoto ametelekezwa au ameendelea kutojaliwa na wazazi;
- (b) wazazi hawawezi kupatikana;
- (c) wazazi hawawezi kutoa ridhaa; au
- (d) ridhaa imezuiliwa na wazazi bila ya sababu ya msingi na mzazi au wazazi wote wawili na malezi ya kambo yameonekana kuwa ni muhimu kwa maslahi bora ya mtoto kwa mujibu wa taarifa ya uchunguzi ya kijamii.

(5) Kamishna ataamua kuhusu malezi ya kambo ndani ya siku thelathini kutoka tarehe ya kupokea taarifa ya uchunguzi wa kijamii ikiwa imeambatishwa na nyaraka nyingine muhimu.

(6) Kamishna anaweza kumweleza Afisa Ustawi wa Jamii kuidhinisha malezi ya kambo endapo masharti ya kanuni ndogo ya (8) yatakuwa yamezingatiwa na ridhaa ya wazazi au walezi imetolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (3).

(7) Afisa Ustawi wa Jamii aliyeelekezwa kuidhinisha malezi ya kambo chini ya kanuni ndogo ya (5) atatoa uamuzi kuhusu malezi ya kambo ndani ya siku thelathini baaada ya kupokea taarifa ya uchunguzi wa kijamii iliyokamilika.

(8) Ndugu waliozaliwa tumbo moja hawatatenganishwa na utaratibu mahsusi utazingatiwa kuwaweka mapacha pamoja.

Taarifa ya
uchunguzi wa
kijamii

9.-(1) Afisa Ustawi wa Jamii atafanya uchunguzi wa kijamii kuhusiana na-

- (a) mtoto ambaye ametambuliwa kwenye maombi ya malezi ya kambo;
- (b) mtoto ambaye ametambuliwa na meneja wa makazi yaliyohibitishwa au taasisi kuwa anastahili kuwekwa kwenye malezi ya kambo;
- (c) mtoto yeyote ambaye ametambuliwa na Afisa wa Ustawi wa Jamii kuwa anastahili kuwekwa kwenye

malezi ya kambo.

(2) Uchunguzi wa kijamii utathmini-

(a) hali ya mtoto na familia ya mtoto;

(b) uwezekano wa kumfanya mtoto kuwa pamoja tena na wazazi wake wa kibailojia na hatua zilizochukuliwa tayari kumrudisha mtoto kwa wazazi wake wa kibailojia;

(c) iwapo mtoto anastahili kuwekwa kwenye malezi ya kambo;

(d) iwapo mzazi wa kambo anastahili kulea mtoto ambaye anahusika na uchunguzi wa kijamii

(3) Taarifa ya uchunguzi wa kijamii itakuwa katika utaratibu uliowekwa kama unavyofanana na Fomu Na. 7 katika Jedwali.

(4) Wakati wa kufanya uchunguzi wa kijamii, Afisa wa Ustawi wa Jamii lazima-

(a) kama mtoto anaweza kujieleza mwenyewe, akutane na mtoto kufahamu maoni yake kama mtoto huyo anaweza kutoa maoni yake na atawajibika kuweka kumbukumbu ya maoni hayo katika taarifa ya uchunguzi wa kijamii;

(b) akutane na wazazi wa mtoto, kuangalia uwezekano wa kumuunganisha tena mtoto kwa wazazi na kusikiliza maoni yao kuhusu kumweka mtoto katika malezi ya kambo;

(c) kuhakikisha maoni ya wazazi wa kambo kuhusu kumlea mtoto ambaye anahusika na taarifa ya uchunguzi wa kijamii.

(5) Endapo wazazi wa mtoto wamefariki au hawawezi kupatikana; Afisa Ustawi wa Jamii lazima apate taarifa ya polisi kuhusu hali ya wazazi.

(6) Afisa Ustawi wa Jamii, katika kutathmini ustahili wa malezi ya kambo, atazingatia maslahi bora ya mtoto kwa kutoa uzito wa kutosha katika maoni ya mtoto kwa kuzingatiwa umri wa mtoto na kupevuka.

(7) Afisa Ustawi wa Jamii kwa wakati muafaka, atakamilisha taarifa ya uchunguzi wa kijamii na kuiwasilisha kwa Kamishna katika utaratibu ulioanishwa kwenye fomu Na. 7 iliyopo kwenye Jedwali.

ambaye anaabudu dini moja na mtoto na endapo mzazi wa kambo dini yake ni tofauti na ya mtoto, mzazi wa kambo atachukua hatua muhimu za kumwezesha mtoto huyo kuwa na haki ya kuabudu kulingana na dhehebu lake.

(2) Pale ambapo dini ya mtoto haifahamiki, mtoto atawekwa kwa mzazi wa kambo ambaye anaweza kumlea kulingana na dhehebu la dini ya mzazi wa kambo.

Majukumu ya
walezi wa
kambo

11.-(1) Mlezi wa kambo, pamoja na majukumu yaliyobainishwa kwenye fomu Na. 6 iliyoko kwenye Jedwali, atakuwa na jukumu la kumpa mtoto mahitaji ya kila siku ikijumuisha:

- (a) kutokuzuia mawasiliano baina ya mtoto wa kambo na ndugu wa kibailojia na watu wengine wenye maslahi katika ustawi na maendeleo ya mtoto isipokuwa kama kuna amri ya katazo la mahakama;
- (b) kushirikiana na Afisa Ustawi wa Jamii ili kuhamasisha kuunganishwa tena kwa mtoto na wazazi wake wa kibailojia ndugu au ndugu wa kibailojia, pale inapowezekana na kama hivyo ni kwa mujibu wa mpango wa malezi uliotayarishwa wakati wa kumweka mtoto kwenye malezi kwa mujibu wa kanuni ya 17 ya Kanuni hizi;
- (c) kuruhusu Afisa Ustawi wa Jamii kutembelea nyumba aliko mtoto ili kufanya tathimini, kwa madhumuni ya kukagua mpango wa malezi ya kambo, kufanya mapitio ya mpango wa malezi au kwa ajili ya jambo jingine lolote kuhusiana na mpango wa malezi ya kambo.
- (d) kuhakikisha mtoto anapata elimu ya msingi na kadri itakavyowezekana apate elimu zaidi na mafunzo kwa kulingana na uwezo wake na fursa zilizopo;
- (e) kuheshimu maoni ya mtoto, na kwa ujumla kuhamasisha ustawi, maslahi na maendeleo ya mtoto kimwili, kihisia na kijamii na pale inaporuhusiwa ushiriki katika mpango wa makazi ya awali na maendeleo ya mtoto;
- (f) kuongoza mwenendo wa mtoto kiutu, kuhamasisha nidhamu chanya na kutokumpa adhabu ya viboko au aina vyingine ya mateso ya mwili au adhabu au unyanyasaji au nidhamu ya kudhalilisha;

- (g) kuhakikisha matunzo ya kiafya yanapatikana, uangalizi wa mtoto na kufuata maelekezo kama yatakavyotolewa na Afisa wa Afya;
- (h) pale ambapo mpango wa malezi ya kambo utatayarishwa kwa mujibu wa masharti ya kanuni ya 17 ya Kanuni hizi, kuzingatia masharti ya mpango huo;
- (i) kahakikisha pale ambapo mtoto anatoka kwenye mazingira tofauti ya kiutamaduni, lugha na dini anasaidiwa kudumisha muungano na utamaduni, lugha na dini yake;
- (j) kuhakikisha kuwa mtoto anatunzwa kwa namna sawasawa na watoto wengine anaishi nao kwenye makazi yaleyale isipokuwa pale ambapo mahitaji maalum ya mtoto huyu au mwingine yeyote kwenye makazi hayo yanataka vinginevyo.

(2) Mtoto aliye chini ya malezi ya kambo hatachukuliwa au kusafiri bila ruhusa ya maandishi ya Kamishna wa Ustawi wa Jamii.

(3) Mzazi wa kambo atamjulisha Afisa Ustawi wa Jamii mabadiliko yoyote ya anwani ya wilaya anayoishi na atatoa notisi ya siku zisizopungua sitini, ya nia ya kuhama kutoka wilaya anayoishi au kwenda nje ya nchi.

(4) Mzazi wa kambo, ndani ya siku ishirini na moja toka kutokea mabadiliko yoyote ya kimaisha atamjulisha Afisa Ustawi wa Jamii kuhusu mabadiliko hayo ya maisha na ataeleza ni kwa namna gani yatamuathiri mtoto.

(5) Mzazi wa kambo hataacha majukumu ya kutunza mtoto wa kambo mikononi mwa mtu mwingine yeyote kwa kipindi cha zaidi ya wiki moja mfulululizo bila ruhusa ya Afisa Ustawi wa Jamii.

(6) Mzazi wa kambo atamjulisha Afisa Ustawi wa Jamii juu ya nia ya kuasili mtoto wa kambo.

Haki za wazazi
wa kambo

12.-(1) Mzazi wa kambo ana haki ya kufanya maamuzi siku hadi siku kuhusu matunzo, malezi na maendeleo ya mtoto wa kambo aliye chini ya uangalizi wake.

(2) Bila ya kujali kanuni ndogo ya (1), wazazi wa kambo watashirikiana na Afisa Ustawi wa Jamii ili kupata maoni ya wazazi wa kibaiolojia kuhusu maamuzi makubwa yenye athari kwa mtoto wa kambo, iwapo itawezekana kupata maoni yao, na

iwapo maoni hayo hayatakuwa kinyume na maslahi ya mtoto, maoni ya wazazi wa kibaiolojia yatapelewa uzito unaostahili katika kufanya maamuzi hayo.

(3) Mzazi wa kambo ana haki ya faragha ya maisha yake ya nyumbani na si kusababishiwa vitisho, manyanyaso na maelekezo yasiyostaiki toka kwa wazazi wa kibaiolojia au ndugu wa mtoto wa kambo juu ya majukumu yake ya malezi ya kambo.

(4) Mzazi wa kambo ana haki ya kufahamishwa na Afisa Ustawi wa Jamii kuhusu ukweli au tukio ambalo linaweza kuleta athari kwenye malezi ya kambo ya mtoto aliye chini ya uangalizi wake. Mzazi wa kambo ana haki ya kuomba kuasili miezi sita baada ya mtoto kuwa chini ya malezi yake kwa mujibu wa Sehemu ya VI ya Sheria.

(5) Mzazi wa kambo ana haki ya ushauri na msaada kuungwa mkono na Afisa Ustawi wa Jamii ili kumwezesha kulea mtoto wa kambo ipasavyo na kushirikiana na wazazi wa kibaiolojia wa mtoto.

(6) Mzazi wa kambo ana haki ya kujulishwa na Afisa ustawi wa Jamii kuhusu maendeleo ya afya ya mtoto wa kambo, ikiwa ni pamoja na kumbukumbu za chanjo, historia ya elimu yake na msaada wa kijamii au wa kisaikolojia ambao ulitolewa ili kuwezesha malezi ya kambo ambayo mtoto wa kambo anahitaji.

Haki za mtoto
wa kambo

13.-(1) Mtoto wa kambo ana haki ya kupata mahitaji ya kila siku kutoka kwa mzazi wa kambo.

(2) Mtoto wa kambo ana haki ya kuendelea kuwasiliana na ndugu zake wa kibaiolojia na watu wengine isipokuwa kama imeamriwa na mahakama au Afisa Ustawi wa Jamii kuwa mawasiliano hayo hayana maslahi kwa mtoto.

(3) Mtoto wa kambo ana haki ya kupata elimu ya msingi, kuhudhuria masomo kila mara kama ametimiza umri wa kwenda shule na kupata elimu ya ya ufundi na kupata elimu ya juu kadri itakavyowezekana.

(4) Mtoto wa kambo ana haki ya kutoa maoni na maoni yake kuheshimiwa katika maamuzi yote yanayomhusu.

(5) Mtoto wa kambo ana haki ya kuwasiliana kwa uhuru na Afisa Ustawi wa Jamii na mamlaka nyingine kuhusu malezi, matunzo na matibabu yake.

Mipango ya
kusaidia wazazi

14.-(1) Afisa Ustawi wa Jamii kwa kadri

wa kambo na
mtoto wa
kambo

inavyowezekana na kwa kushirikiana na shirika jingine lolote atamsaidia Mzazi wa kambo kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa ya maandishi inayoelezea malezi ya kambo, mahitaji ya kisheria ya malezi hayo, haki za kisheria za wazazi wa kambo, mtoto wa kambo na wazazi wa kibailojia na pia kutoa mafunzo juu ya mahitaji ya kisaikolojia na kijamii ya mtoto wa kambo na ushauri nasaha wakati wa malezi ya kambo.

(2) Afisa Ustawi wa Jamii atasaikia na kutoa ushauri nasaha ili kumwezesha mtoto wa kambo kuzoea kuishi kwenye malezi ya kambo.

(3) Afisa Ustawi wa Jamii atatoa ushauri nasaha kwa mtoto wa kambo iwapo kutatoka kusitishwa malezi ya kambo na iwapo kutakuwa na notisi ya kusitishwa huko, ushauri nasaha utatolewa mapema ili kumuandaa mtoto kwa ajili ya kuhama huko.

(4) Pale ambapo malezi ya kambo yanakaribia kukoma kwa sababu ya mtoto kutimiza miaka kumi na nane, Afisa Ustawi wa Jamii atamsaidia mtoto wa kambo kutafuta makazi na ajira au kuendelea na masomo au mafunzo ya ufundi na atashirikiana na mzazi wa kambo kutoa ushauri ili kumuandaa mtoto na kusitishwa kwa malezi ya kambo na kuanza maisha ya kujitegemea.

Mipango ya
kiafya

15.-(1) Isipokuwa katika hali ya dharura, mtoto atakuwa chini ya uangalizi wa mzazi wa kambo hadi awe amefanyiwa vipimo na mtaalam wa afya na taarifa ya maandishi kuhusu hali ya mtoto kimwili na kiakili kupelekwa kwa Afisa Ustawi wa Jamii.

(2) Katika hali ya dharura taarifa ya vipimo chini ya kifungu kidogo (1) cha kanuni hii itatolewa ndani ya wiki nne baada kuanza malezi ya mama wa kambo.

(3) Wakati malezi ya kambo yatakapoanza, Afisa Ustawi wa Jamii atatoa taarifa kwa wazazi wa kambo orodha ya chanjo zilizotolewa kwa mtoto wa kambo na kuonyesha orodha ya chanjo nyinginezo zitakazotolewa kwa mujibu wa ratiba ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, na mzazi wa kambo atahakikisha kwamba chanjo hizo zinatolewa.

(4) Mzazi wa kambo na Afisa Ustawi wa Jamii watatunza kwa nyakati zote kumbukumbu za chanjo za mtoto wa kambo.

(5) Pale ambapo mtoto wa kambo aliye chini ya umri wa miaka mitano atakuwa kwenye uangalizi wa mzazi wa kambo:

- (a) mzazi wa kambo atahakikisha kuwa mtoto wa kambo amepimwa afya na mtaalamu kama ilivyotajwa kwenye kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii na upimaji afya utafanyika mwezi mmoja baada ya malezi ya kambo kwanza na baadaye mara moja kila baada ya miezi sita; na Afisa Ustawi wa Jamii muhusika wa malezi ya kambo atasaidia kadri inavyowezekana kuwezesha mzazi wa kambo kuhakikisha matakwa ya kanuni hii ndogo yanayotekelezwa; na
- (b) mzazi wa kambo atahakikisha mtoto wa kambo anahudhuria kliniki kila mwezi.
- (2) Pale ambapo mtoto wa kambo aliye na umri wa zaidi ya miaka mitano yuko chini ya mzazi wa kambo, mtoto huyo atafanyiwa vipimo vya afya na mtaalamu aliyetajwa kwenye kanuni ndogo (1) mara moja kila baada ya miezi sita.
- (3) Daktari ambaye anampima mtoto wa kambo kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2), (5) au (6) ya Kanuni hii atatoa taarifa ya maandishi kwa Afisa Ustawi wa Jamii ambaye mtoto wa kambo aligundua hali yake ya kimwili, kiakili na kihisia kwa utaratibu uliowekwa kama unavyofanana na Fomu Na.8 katika Jedwali.
- (4) Endapo mtoto wa kambo ni mgonjwa. Mzazi wa kambo atahakikisha mtoto huyo anafanyiwa vipimo vya kitabibu na kutibiwa mapema iwezekanavyo, iwapo mtoto atabainika kuwa na mgonjwa unaotishia uhai wake basi mzazi wa kambo atawasilisha taarifa kwa Afisa Ustawi wa Jamii ndani ya saa 24 za vipimo husika naye Afisa Ustawi wa Jamii atawajulisha Wazazi au Walezi wa mtoto wa kambo.

Ziara za
ukaguzi katika
malezi ya
kambo

16.-(1) Afisa Ustawi wa Jamii atatembelea familia ya kambo katika makazi yao na kumuona mtoto wa kambo:

- (a) ndani ya wiki mbili baada ya tarehe ya kwanza malezi ya kambo ambapo mtoto wa kambo ana umri chini ya miaka miwili na baadaye mara moja kwa kila miezi miwili;
- (b) ndani ya mwezi mmoja baada ya tarehe ya kuanza malezi ya kambo ambapo mtoto wa kambo ana umri wa zaidi ya miaka miwili na baadaye mara moja kila miezi miwili;
- (c) mara tu kutakapokuwa na taarifa za unyanyasaji wa

mtoto, na katika mazingira ya namna hiyo kutembelea mtoto kutafanyika kwa mujibu wa kifungu cha 96 cha sheria; na

- (d) si zaidi ya wiki moja baada ya kupokea taarifa toka kwa mtoto, mzazi wa kambo au mtu mwingine yeyote inayoonyesha kuwa kuna umuhimu wa kumtembelea mtoto.

(2) Afisa Ustawi wa Jamii atakutana na mtoto katika faragha wakati akimtembelea pale ambapo mtoto atakuwa na uwezo wa kujieleza, ili kuweza kupata maoni yake kuhusu malezi ya kambo na matunzo.

(3) Afisa Ustawi wa Jamii anayemtembelea mtoto kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii atatayarisha taarifa ya maandishi ikieleza alichobaini kuhusiana na maendeleo, mwenendo na mabadiliko yoyote yaliyotokea katika Familia ya kambo; na taarifa hiyo itawekwa kwenye jalada la mtoto.

(4) Taarifa iliyotayarishwa chini ya kanuni ndogo ya (3) itajumuisha maelezo juu ya maoni ya mtoto na hisia zake kuhusiana na malezi, matunzo na matibabu kama ilivyoainishwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2).

(5) Baada ya ziara kwa mujibu wa kanuni hii Afisa Ustawi wa Jamii atagundua kuwa kuna mabadiliko katika mazingira ya malezi ya kambo kwa kiasi kwamba kuna athari hasi kwa mtoto wa kambo au malezi ya kambo hayana maslahi bora kwa mtoto, Afisa huyo atazingatia kusitishwa kwa malezi kwa mujibu wa kanuni ya 18 ya Kanuni hizi.

(6) Bila kujali kanuni ndogo ya (5) Afisa Ustawi wa Jamii anaweza ongeza msaada na ushauri kwa mzazi wa kambo na mtoto wa kambo, pia anaweza kuongeza ziara pale ambapo ataona kuwa kufanya hivyo kutaweza kutatua matatizo yoyote yaliyobainika wakati wa ziara kwenye malezi ya kambo.

(7) Kamishna ataandaa mwongozo na fomu za kuchukulia na kutolea taarifa kuhusiana na ziara za usimamizi wakati wa malezi ya kambo.

Mpango wa
malezi ya
kambo

17.-(1) Kuanzia wakati mtoto atakapokuwa kwa mzazi wa kambo, kipaumbele kitatolewa kwa maisha ya baadae ya mtoto wa kambo na msaada unaohitaji kumuandaa mtoto wa kambo kwa ajili ya uangalizi wa kudumu, ikijumuisha, kumunganisha tena mtoto na mzazi wake wa kibaiolojia, na kwa azma hiyo Afisa Ustawi wa Jamii atatayarisha mpango wa malezi

ya kambo kwa kila mtoto aliye chini ya malezi ya kambo.

(2) Mpango wa malezi ya kambo utatayarishwa kabla ya malezi hayo na kwa uchache:

- (a) utaainisha sababu za mpango wa malezi ya kambo;
- (b) utaainisha taarifa kuhusu afya ya mtoto mahitaji, elimu na historia yake ya kijamii na kisaikolojia;
- (c) utaainisha misaada ambayo Afisa Ustawi wa Jamii atatoa kwa mtoto wa kambo na mzazi wa kambo ili kuwezesha malezi ya kambo;
- (d) pale ambapo kuna uwezekano wa kuwaunganisha wazazi wa kibailojia, iwekwe bayana ni hatua zipi zitachukuliwa kuhamasisha muungano wa mtoto wa kambo na wazazi wa kibailojia;
- (e) utaweka bayana aina ya mawasiliano ambayo mtoto wa kambo atakuwa nayo na familia yake ya kibailojia; na
- (f) ziainishwe njia mbadala za malezi ya kambo ya kudumu ikiwa ni pamoja na kuasiliwa na wazazi wakambo, iwapo itabainika kwamba mtoto hawezi kuunganishwa tena na familia yake ya kibailojia.

(3) Afisa Ustawi wa Jamii atapitia na kuhuisha upya mpango wa malezi ya kambo kila baada ya miezi miwili kama sehemu ya ziara za mara kwa mara kama inavyoelekezwa na kanuni ya 16 ya Kanuni hizi ili kuhakikisha kuwa mpango wa malezi ya kambo unaendelea kukidhi mahitaji ya mtoto wa kambo.

(4) Mpango wa malezi ya kambo utatayarishwa na kufanyiwa mapitio kwa kushauriana na:

- (a) mtoto wa kambo, ambapo atatoa maoni yake;
- (b) mzazi wa kambo; na
- (c) wazazi wa kambo pale ambapo inawezekana na si kinyume na maslahi bora ya mtoto.

(5) Kamishna atatarisha mwongozo, taratibu na fomu kwa ajili ya mpango wa malezi ya kambo kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1).

Kusitisha kwa
Malezi ya kambo

18.-(1) Afisa Ustawi wa Jamii atasitisha malezi ya kambo katika mazingira yafuatayo:

- (a) pale ambapo amepieleza masuala ya ulinzi wa mtoto kwa mujibu wa kifungu cha 96 cha Sheria na kubaini kuwa mtoto amenyanyaswa au anahitaji

malezi na ulinzi na amemuondoa mtoto;

- (b) pale ambapo kwa mujibu wa Afisa Ustawi wa Jamii mtoto anaweza kuunganishwa na wazazi wake wa kibailojia au familia;
- (c) pale ambapo kwa amri mtoto aliwekwa kwenye malezi ya kambo au malezi ya muda chini ya kifungu cha 18 cha sheria ya amri hiyo imefikia ukomo; au
- (d) pale ambapo Afisa Ustawi wa Jamii ataona kuwa malezi ya kambo hayana maslahi bora kwa mtoto na kwamba malezi mbadala ya kambo yanahitajika kwa mtoto.

(2) Afisa Ustawi wa Jamii atatathmini maoni ya mtoto wa kambo pale ambapo mtoto anaweza kujieleza, na maoni hayo yatapewa Uzito kwa kuzingatia umri na ukomavu wa mtoto, katika kuamua kusitisha malezi ya mtoto chini ya kanuni ndogo ya 1 (b) na (d).

(3) Afisa Ustawi wa Jamii ataweka kwenye jalada la mtoto kumbukumbu ya kilichosababisha usitishwaji wa malezi ya kambo na maoni ya mtoto wa kambo kuhusu usitishwaji huo.

(4) Pale ambapo malezi ya kambo yatasitishwa chini ya kanuni ndogo (1) (b), (c) na (d), Afisa Ustawi wa Jamii atamjulisha mzazi wa kambo juu ya uamuzi wa kusitisha malezi ya kambo na atamjulisha mtoto wa kambo kwa kuzungumza katika namna ambayo mtoto anaweza kuelewa, siku kumi kabla ya kusitishwa malezi ya kambo.

(5) Pale ambapo kutatokea kufunga au kuvunjika ndoa ya mzazi wa kambo Afisa Ustawi wa Jamii:

- (a) atafanya tathmini kubaini kama malezi ya kambo yanayoendelea yana maslahi kwa mtoto;
- (b) atafanya tathmini juu ya mwenzu wa mzazi wa kambo ili kubaini kama wanafaa kuwa walezi kwa mujibu wa kanuni ya 6 ya Kanuni hizi, ni iwapo mzazi wa kambo ambaye alipewa jukumu la kulea akiwa bado hajafunga ndoa ataamua kuoa ua kuolewa; na
- (c) atasitisha malezi ya kambo kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) (d), kama atabaini kuwa kwa kuzingatia tathmini iliyofanyika, malezi hayo hayana tena maslahi kwa mtoto.

(6) Ikiwa Afisa Ustawi wa Jamii atachukua uamuzi wa kusitisha malezi ya kambo chini ya kanuni ndogo ya (1) (d), na

mtoto amekuwa chini ya uangalizi wa mzazi wa kambo katika kipindi cha miezi sita kwa uchache, na mzazi wa kambo anaamini kuwa kusitishwa kwa malezi ya kambo hakutakuwa na maslahi kwa mtoto, mzazi wa kambo anaweza kukata rufaa kimaandishi na kuiwasilisha kwa Kamishna ndani ya siku kumi tangu uamuzi kufikishwa kwa mzazi wa kambo na atamjulisha Afisa Ustawi wa Jamii juu ya kuwasilishwa kwa rufaa hiyo.

- (a) kwa ajili ya rufaa, Afisa Ustawi wa Jamii atawasilisha nakala ya jalada la mtoto ambalo linajumuisha sababu za uamuzi wa kusitisha malezi ya kambo kwa Kamishna ili aweze kulipitia;
- (b) kamishna atafanya uamuzi juu yauwezekano wa kusitisha malezi ya wazazi wa kambo na Afisa Ustawi wa Jamii ndani ya siku kumi na tano baada ya kupokea rufaa;
- (c) mtoto wa kambo ataondolewa kwa Mzazi wa kambo mpaka Kamishna atakapofanya uamuzi na kuamua kuwa malezi ya kambo yasitishwe.

(7) Mtoto wa kambo atakapotimiza umri wa miaka kumi na nane anaweza akaondoka chini ya malezi ya kambo.

(8) Mtoto wa kambo aliyetimiza miaka kumi na nane lakini bado anaendelea na masomo ya kawaida au ya ufundi anaweza kubaki kwenye malezi atakapotimiza umri wa miaka ishirini na moja.

(9) Itakapowasilishwa notisi ya kwamba mzazi wa kambo anataka kuhama makazi yake kwa mujibu wa kanuni ya 11(3), Afisa Ustawi wa Jamii atafanya tathmini juu ya kama mtoto anataka kukaa na mzazi wa kambo na tathmini hii itafanywa ndani ya siku thelathini baada yakupokea notisi hiyo.

(10) Katika kufanya tathmini inayohitajika katika kanuni ndogo ya (4), Afisa Ustawi wa Jamii atazingatia matamania na uwezekano wa kumuunganisha tena mtoto kwa wazazi wake wa kibailojia, lakini pia maslahi ya mtoto, maoni ya mtoto na kama anaweza kutoa maoni yake basi yatazingatiwa na kupewa umuhimu kulingana na umri na ukomavu wa mtoto.

(11) Pale ambapo itaamuliwa kwamba mtoto akae na Wazazi wake wa kambo, Afisa Ustawi wa Jamii wa wilaya anayotoka atahamisha nyaraka zote husika kwa Afisa Ustawi wa Jamii wa wilaya mpya na Afisa Ustawi wa Jamii ataweka kumbukumbu katika rejesta ya malezi ya kambo ipasavyo.

(12) Kamishna atatararisha mwongozo, taratibu na fomu

zitakazohusu usitishwaji wa malezi ya kambo.

Kifo

19.-(1) Iwapo mtoto wa kambo atafariki, mzazi wa kambo atamjulisha Afisa Ustawi wa Jamii ndani ya saa ishirini na nne tangu kufariki kwa mtoto wa kambo, Afisa Ustawi wa Jamii ambaye atamjulisha Kamishna mara moja.

(2) Kufuatia kifo cha mtoto wa kambo, mzazi wa kambo kwa kushauriana na Afisa Ustawi wa Jamii atafanya juhudi zote ili apate cheti cha kifo cha mtoto na taarifa ya uchunguzi wa sababu za kifo ambayo itawasilishwa kwa Kamishna na Afisa Ustawi wa Jamii.

(3) Pale ambapo wazazi au walezi wa mtoto wanafahamika, Kamishna atawajulisha juu ya kufariki kwa mtoto ndani ya saa ishirini na nne baada ya kupokea taarifa hizo.

(4) Iwapo mzazi wa kambo atafariki, kama mtoto alikuwa chini ya malezi ya mzazi mmoja wa kambo, ikiwa wazazi wote wawili watafariki, Afisa Ustawi wa Jamii atapanga malezi ya kambo mbadala mara moja.

Makosa

20.-(1) Mtu atakayekiuka sharti lolote la Kanuni hizi anatenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni moja au isiyozidi shilingi milioni tatu au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au vyote viwili na kulipa shilingi elfu hamsini kwa kila siku ambayo kosa linaendelea kutendeka.

—
JEDWALI
—

Kanuni za Malezi ya Kambo

FOMU

SHERIA YA MTOTO
KANUNI ZA MALEZI YA KAMBO ZA MWAKA, 2011
(TANGAZO LA SERIKALI NA. LA 2011)

F.C. Fomu Na. 1

MAOMBI YA KUWA MLEZI WA KAMBO

Kanuni ya 4(1)

1. **Taarifa za mwombaji/waombaji**

1.1. Je ni maombi ya pamoja au binafsi?
PAMOJA/BINAFSI

Futa isiyohusika

1.2. **Mwombaji 1**

Mwombaji 2

1.3. Jina:

.....

1.4. Tarehe ya kuzaliwa:

.....

1.5. Jinsi:

.....

1.6. Hali ya ndoa:

.....

1.7. Utaifa:

.....

1.8. Kazi:

.....

2. **Anwani**

2.1. Wilaya:

2.2. Kata

.....

.....

2.3. Anwani ya Makazi:

.....

2.4. Anwani ya posta:

.....

2.5. Simu:

.....

2.6. Simu ya mkononi (Mwombaji 1/Mwombaji 2):

.....

2.7. Barua pepe: (mwombaji 1/Mwombaji 2):

.....

Kanuni za Malezi ya Kambo

3. Wanafamilia wengine

3.1. Toa taarifa za watoto **wote** waliochini ya uangalizi wako:

Jina	Jinsi	Tarehe ya kuzaliwa	Uhusiano Na Mwombaji/Waombaji	Kiwango cha Elimu
—	—	—	—	—
—	—	—	—	—
—	—	—	—	—
—	—	—	—	—
—	—	—	—	—

3.2. Toa taarifa za watu wengine **wowote** wanaoishi **kwenye** makazi yako:

Jina	Jinsi	Tarehe ya kuzaliwa	Uhusiano Na Mwombaji/Waombaji	Kazi
—	—	—	—	—
—	—	—	—	—
—	—	—	—	—

4. Taarifa za malezi ya kambo

4.1. Kwa nini unataka kuwa mlezi wa kambo?

.....

.....

4.2. Je umeshawahi kulea mtoto wa kambo? (Kama ni NDIYO toa **maelezo** chini):

NDIYO/HAPANA

Futa isiyohusika			
Jina	Jinsi	Tarehe ya kuzaliwa	Mazingira yaliyosababisha kusitisha malezi (kama malezi yamesitishwa)
—	—	—	—
—	—	—	—
—	—	—	—

4.3 Je **uliwahi kuomba** kuwa mlezi wa kambo **ukakataliwa**? **NDIYO/HAPANA**

Futa isiyohusika

Kama NDIYO, toa maelezo:

.....
.....

4.4. Je maombi ya ulezi wa kambo ni ya jumla au ni ya mtoto mahususi? (JUMLA/MAHSUSI)

4.5 Futa kama inafaa

4.6. Kama maombi ni kwa ajili ya mtoto mahususi (Jina kamili na mahali anapoishi):

.....

4.7. Kama maombi ni ya ujumla, ni watoto wa namna gani unahitaji kuwalea?

Jinsi	Kundi rika	Mahitaji maalum- (Watoto wenye ulemavu (ainisha ni yapi) kudumu, UKIMWI, VVU n.k).
.....		

5. **Weka wazi kuhusu kutiwa hatiani**

5.1. Je yupo mtu yeyote katika kaya ambaye amewahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai?
NDIYO/HAPANA

Futa isiyohusika

(kama NDIYO toa taarifa ikijumuisha majina na tarehe)

Tarehe	Jina	kosa
.....		
.....		

6. Wadhamini

- 6.1. Toa maelezo ya wadhamini WATATU hapo chini ambao wanakufahamu kwa miaka isiyopungua miaka mitatu, Angalau mmoja wapo awe ndugu wa karibu, Mwenyekiti wako wa Kijiji/Mtaa au jirani.

Jina	Nafasi/uhusiano na mwombaji	Taarifa za mawasiliano
_____	_____	_____
_____	_____	_____
_____	_____	_____

7. Tamko

Mimi/sisi (futa isiyohitajika) nathibitisha/tunathibitisha kwamba tunaomba kuwa walezi wa kambo na taarifa zilizotolewa katika fomu hii ni za kweli na sahihi kwa kadri ya ufahamu wangu/wetu.

7.2. Mwombaji 1	Mwombaji 2
Saini _____	_____
Jina _____	_____
Tarehe _____	_____

Kanuni za Malezi ya Kambo

SHERIA YA MTOTO

KANUNI ZA MALEZI YA KAMBO ZA MWAKA, 2011

(Tangazo la Serikali Na.....la mwaka 2011)

Fomu Na. 2

TATHMINI YA MWOMBAJI KUWA MLEZI WA KAMBO

Kanuni ya 6(4)

1. Chanzo cha taarifa. (Ainisha vyanzo vyote vya taarifa katika kufunya tathimini, na kama inahusika tarehe).

1.1. Tarehe ya ziara ya kutembelea makazi(tarehe)

1.2. Tarehe ya kukutana na Mwombaji(tarehe)

1.3. Majadiliano na watoto wa Mwombaji kama wapo (tarehe)

1.4. Tarehe ya kukutana na Daktari(tarehe)

1.5. Maelezo ya wadhamini (jina, nafasi na uhusiano na mwombaji):

1.

2.

3.

4.

5.

6.

7.

8.

1.6. Mengineyo (toa maelezo)

Jina

Tarehe

2. Taarifa za Mwombaji /Waombaji

2.1. Je ni maombi ya pamoja au binafsi
PAMOJA/BINAFSI

❖ Futa isiyohitajika

2.2. Mwombaji 1

Mwombaji 2

2.3. Jina

2.4. Tarehe ya kuzaliwa

2.5. Jinsi

2.6. Utaifa

2.7. Kazi

2.8. Hali ya ndoa

2.9. Dini

2.10. Aina ya ndoa (Kwa maombi ya pamoja)

(Mke mmoja / wake wengi)

❖ Futa isiyohitajika

2.11 Je maelezo ya makazi yaliyotolewa katika maombi ya mwombaji kuwa mzazi wa kambo ni sahihi na yanajitosheleza? NDIYO /HAPANA.

2.12. Futa isiyohitajika.

Kama HAPANA, Tafadhali toa maelezo rekebisha maombi kama inavyotakiwa

.....

.....

.....

3. Mazingira ya mwombaji

Kanuni za Malezi ya Kambo

3.1. Eneo la makazi ya mwombaji

3.2. Wilaya:

Kata

.....

.....

3.3. Toa maelezo ya nyumba ya mwombaji:

.....

.....

Idadi ya vyumba vya kulala Aina ya choo.....

3.4. Aina ya maji yanayotumika.....

3.5. Chanzo kikuu cha mapato ya Mwombaji.....

3.6. Toa maelezo kuhusu biashara au shamba linalomilikiwa na mwombaji

3.7. Je mwombaji/waombaji msaada wowote wa kumwezesha kulea mtoto wa kambo?

NDIYO/HAPANA

Futa isiyohusika

Kama NDIYO toa maelezo

3.8. Je kuna masuala yanayohusu malezi ya mtoto yanayotokana na tathimini au masuala yaliyobainishwa na watoto (kama wapo ndani ya kaya) yanayoweza kuathiri mtoto wa kambo anayehusika?

NDIYO/HAPANA

Futa isiyohusika

Kama NDIYO toa ufafanuzi

.....

.....

3.9. Je mwombaji ana ulemavu au ugonjwa ambao unaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa uwezo wake wa kumlea mtoto wa kambo au mtu yeyote anayeishi katika kaya hiyo ana matatizo yoyote ya afya ya akili yanayoweza kuleta madhara kwa mtoto wa kambo?

NDIYO/HAPANA

Futa isiyohusika

Kama NDIYO, toa ufafanuzi:

.....

.....

3.10. Je mwombaji/ waombaji au mwanafamilia wa kaya ameshawahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai:

NDIYO/HAPANA

Kanuni za Malezi ya Kambo

Futa isiyohusika

Kama NDIYO, toa ufafanuzi (ukijumuisha kutaja kosa mahususi la unyanyasaji, udhalilishaji kiasi cha kuathiri ustahili wa mwombaji kuwa mlezi wa kambo):

.....
.....

Kama NDIYO, Je unaamini kuwa yanauzito kiasi cha kufanya maombi ya kuwa mlezi wa kambo yasikubaliwe?

NDIYO/HAPANA

Futa isiyohusika

4. MUHUTASARI WA TATHIMINI YA MAOMBI YA MALEZI YA KAMBO

4.1. Je ni kwa nini waombaji wanataka kuwa walezi wa kambo?

.....

4.2. Je wanafahamu kusudi la malezi ya kambo na makazi ya muda?

NDIYO/HAPANA

Futa isiyohusika

4.3. Ni nini tathimini yako kuhusu ustahili wa mwombaji kuwa mlezi wa kambo? (Toa sababu kwa kurejea matokeo ya safari na mazungumzo na mwombaji/ waombaji, watoto wao, na kwa kuhusianisha na matokeo ya safari na mazungumzo na mtu mwingine mwenye ufahamu katika suala husika).

ANAFAA/HAFAI

Futa isiyohusika

.....
.....
.....

4.4. Kama ANAFAA ni aina gani ya watoto ambayo mwombaji anastahili kuwalea?

Jinsi: MME/KE/YEYOTE Umri:

.....

4.5. Kama ANAFAA, Je waombaji wanaweza kumlea mtoto mwenye ulemavu, magonjwa ya kudumu au hali nyingine inayohitaji uangalizi mahsusi?

NDIYO/HAPANA

(Futa isiyohusika)

Kama NDIYO, toa ufafanuzi:

.....
.....

5. TAMKO NA MAAMUZI

5.1. Mimi ninathibitisha kwamba nimekamilisha tathimini ya maombi yaliyowasilishwa na muhusika/wahusika waliotajwa hapo juu na NINAPENDEKEZA / SIPENDEKEZI (FUTA ISIOYOHUSIKA) kwamba wanaweza kukubaliwa kwenye orodha ya walezi wa kambo waliothibitishwa.

Saini

Jina

Tarehe

.....

Kamishna wa Ustawi wa Jamii

5.2. NAIDHINISHA/SIIDHINISHI (Futa isiyohusika) maombi yaliyowasilisha na mtu binafsi/watu binafsi walioorodheshwa hapo juu kwa ajili ya kujumuishwa katika orodha ya walezi wa kambo walioidhinishwa.

Saini

Tarehe

.....

Kamishna wa Ustawi wa Jamii

SHERIA YA MTOTO

KANUNI ZA MALEZI YA KAMBO ZA MWAKA, 2011

(Tangazo la Serikali Na..... la mwaka 2011)

F.C. Fomu Na. 3

REJESTA YA WALEZI WA KAMBO

Kanuni ya 7(1)

Namba ya mlezi	Jina la mlezi wa kambo			Tarehe ya kuzaliwa	Jinsi	Hali ya ndoa	Utaifa	Dini	Taarifa za Uandikishaji				Namba ya malezi ya kambo		
	La kwanza	La kati	La mwisho						Wilaya	Tarehe ya kukubaliwa	Tarehe ya kuondolewa			Sababu za kuondolewa	

SHERIA YA MTOTO

KANUNI ZA MALEZI YA KAMBO ZA MWAKA, 2011

(Tangazo la Serikali Na..... la mwaka 2011)

F.C. Fomu Na. 4

REJESTA YA MLEZI WA KAMBO

Kanuni ya 7(7)

Namba ya malezi ya kambo	Taarifa za mtoto					Jinsi	Taarifa za mlezi wa kambo				Taarifa za makazi ya kambo			
	Namba	Jina la kwanza	Jina la kati	Jina la mwisho	Tarehe ya kuzaliwa		Namba	Jina la kwanza	Jina la kati	Jina la mwisho	Wilaya	Tarehe ya kuanza	Tarehe ya mwisho	Sababu za kusitisha

SHERIA YA MTOTO

KANUNI ZA MALEZI YA KAMBO 2011
(TANGAZO LA SERIKALI NA. ...LA 2011)

UTHIBITISHO WA WAZAZI WA KAMBO

Kanuni ya 8 (2) (c)

F.C. Fomu Na. 5

Mimi/Sisi (Jina la mlezi wa kambo 1)

na (Jina la mlezi wa kambo 2)

wa (Anwani kamili ikijumuisha anwani ya mtoto wa kambo)

Nina/tunampokea katika nyumba yangu/yetu (Jina la mtoto wa kambo)

Aliyezaliwa Mnamo

Na zaidi tunakubali:

1. Kutoa malezi ya muda na upendo kwa huyu mtoto kuwa nitampa/tutampa mtoto wa familia yangu/yetu hadi wakati ambao ataunganishwa tena na familia au kuasiliwa kwa mtoto wa kambo kutakapopangwa.
2. Kuchukua majukumu kamili ya malezi na uangalizi ya mtoto huyu kama ambavyo ningefanya/tungefanya kwa mtoto wa familia yangu/yetu.
3. Kutoa malezi yote ya lazima kiafya na matunzo kwa mtoto huyu na kufuata maelezo kama itakavyoelezwa na Daktari.
4. Kutoa elimu na mafunzo kwa mtoto huyu kulingana na uwezo wake na kwa fursa zilizopo kwake nchini.
5. Kukubali mwongozo na usimamizi wa Afisa Ustawi wa Jamii katika malezi yetu na mipango kwa ajili ya mtoto huyu, na kushirikiana na Maafisa Ustawi wa Jamii ambao watapewa jukumu la kufanya kazi nami/nasi.
6. Kumjulisha Afisa Ustawi wa Jamii matatizo yoyote mahsusi ambayo yanaweza kutokea kuhusiana na mtoto na mabadiliko yoyote katika mazingira yangu/yetu ambayo huyo, yanaweza malezi na usalama wa mtoto huyu.

7. Kumshauri Afisa Ustawi wa Jamii kuhusiana na mabadiliko yoyote ya anwani ili waweze kujua kwa nyakati zote alipo mtoto kwa ajili ya kutaza taarifa kama zitakazoweza kuhitajika.

Mlezi wa kambo (1)

Saini:

Jina :

Tarehe:

Mlezi wa kambo (2)

Saini:

Jina:

Tarehe:

Imeshuhudiwa na

Saini :

Jina:

Tarehe:

Imeshuhudiwa na

Saini:

Jina:

Tarehe:

Imeshuhudiwa na

Saini ya shahidi

Jina la shahidi

Wadhifa

Imeshuhudiwa na

Saini ya shahidi

Jina la shahidi

Wadhifa

Kanuni za Malezi ya Kambo

SHERIA YA MTOTO

KANUNI ZA MALEZI YA KAMBO 2011
(TANGAZO LA SERIKALI NA. ...LA 2011)

F.C. Fomu Na. 6

RIDHAA YA WAZAZI AU WALEZI

Kanuni ya 8(3)

Katika shauri la: (Jina la mtoto)

Aliyezaliwa Mnamo
(nakala ya cheti cha kuzaliwa yaweza kuhitajika na taarifa ya polisi inaweza kuhitajika katika mazingira fulani kuthibitisha hadhi ya wazazi)

Mimi/Sisi, nikiwa BABA/MAMA/MLEZI KISHERIA (Futa isiyotakiwa) wa mtoto aliyetajwa hapo juu na kwa kuwa siwezi kutoa matunzo ya mtoto huyu ndani ya familia yetu, nakubali na kuridhia mtoto aliyetajwa hapo juu awewe kwenye malezi ya kambo ambavyo yatakuwa yameidhihinishwa na Kamishna wa Ustawi wa Jamii. Zaidi tunampa mamlaka Kamishna wa Ustawi wa Jamii au Wakala wake aidhinisha matibabu ya kiafya na upasuaji kwa mtoto aliyetajwa hapo juu kama itakavyopendekezwa na Afisa wa afya.

Mzazi /Mlezi (1)

Saini:
Jina :
Uhusiano na mtoto

Imeshuhudiwa na

Saini ya shahidi
Jina la shahidi
Tarehe

Mzazi /Mlezi (2)

Saini
Jina
Uhusiano na mtoto

Imeshuhudiwa na

Saini ya shahidi.....
jina la shahidi
tarehe

Kanuni za Malezi ya Kambo

SHERIA YA MTOTO

KANUNI ZA MALEZI YA KAMBO 2011
(TANGAZO LA SERIKALI NA. ...LA 2011)

F.C. Fomu Na. 7

TAARIFA YA UCHUNGUZI WA KIJAMII *Kanuni ya 9 (1)*

1. Maelezo ya mtoto

1.1 Jina la kuzaliwa Jina la kati Jina la mwisho

.....

1.2 Tarehe ya kuzaliwa 1.3 Jinsi

1.4 Dini 1.5 Kabila

1.6 Mahali anapoishi kwa sasa maelezo ya mawasiliano

.....
.....
.....

2. Vyanzo cha taarifa (ainisha vyanzo vyote vya taarifa vilivyotumika katika kufanya tathmini hii, pale ambapo inahusiana na tarehe.

2.1 Majadiliano na mtoto (tarehe)

2.2 Majadiliano na mzazi /wazazi/mlezi/walezi wa mtoto
(tarehe)
(ainisha nani):

.....

2.3 Majadiliano/mkutano na Polisi (tarehe)

2.4 Majadiliano/mkutano na Afisa wa afya (tarehe)

2.5 mengineyo (toa maelezo)

3. Familia ya sasa /Hali ya malezi

3.1 Ni nini hadhi ya sasa ya wazazi wa mtoto?

Baba: HAI/ AMEFARIKI/HAIJULIKANI (HAYUPO)

Mama: HAI/ AMEFARIKI/HAIJULIKANI (HAYUPO)

3.2 Ni nini hadhi ya ndoa ya wazazi wa mtoto?

3.3 Ni nini mipango ya sasa ya malezi ya mtoto?

4. Mahitaji ya mtoto

4.1 Je mtoto kwa sasa anahudhuria shule/ mafunzo?NDIYO /HAPANA

4.2 Je nmtoto ana mahitaji maalum yoyote ya kielimu

4.3 Je mtoto ana ulemavu, ugonjwa wa kudumu au hali nyingine ambayo inahitaji malezi maalum? NDIYO? HAPANA kama NDIYO, toa maelezo
.....

5. Kuunganishwa tena na familia

Kanuni za Malezi ya Kambo

5.1. Je mtoto ametenganishwa na wazazi wake? NDIYO/HAPANA

Kama NDIYO, kwa muda gani?

5.2. Ni juhudi gani zimefanywa kutafuta wazazi/ kuunganishwa mtoto?

.....

5.3 Ni nini tathimini yako kuhusu uwezekano wa kuunganishwa tena na familia?

.....

6. Tathimini ya malezi ya kambo?

6.1 Ni nini tathimini yako kuhusu sifa ya mtoto kwa ajili ya malezi ya kambo?

.....

6.2 Je umeweza kubainisha walezi wa kambo kwenye sifa? NDIYO/HAPANA

Kama NDIYO, toa maelezo (Walezi wote wa kambo wataidhinishwa na kuingizwa kwenye rejesta - tumia fomu ya maombi (Fomu 1) na Taarifa ya Ustawi wa Jamii (Fomu 2) kwa dhumuni hili.

Majina: Na:

6.3 kwa nini unaamini walezi wa kambo waliopendekezwa wanafaa kwa mtoto huyu ?

.....

6.4 Ni nini maoni ya mtoto?

.....

6.5 Ni nini maoni ya walezi wa kambo wanaotarajiwa?

.....

6.6 . Ni nini maoni ya wazazi wa kibailojia (pale inapotakiwa)

.....

6.7 Je wazazi wa kibailojia au walezi wametoa ridhaa yao kwa ajili ya malezi ya kambo?
NDIYO/HAPANA

Kanuni za Malezi ya Kambo

6.8 Kama HAPANA, eleza sababu ya kuachwa kwa maoni ya wazazi wa kibailojia au walezi kuhusu malezi ya kambo (kwa mujibu wa kanuni 8(4)):

.....

6.9 Je kuna mahitaji yoyote ya matunzo kwa ajili ya malezi ya kambo? NDIYO /HAPANA kama NDIYO, toa maelezo ya matunzo na ni nani atatoa matunzo hayo:

.....

.....

6.10 Ni hatua gani zinatakiwa ili kufanikisha kupatikana malezi ya kudumu ya muda mrefu kwa mtoto huyu?

.....

.....

.....

7. Mapendekezo na maamuzi rasmi

7.1 Nathibitisha kwamba nimehitimisha uchunguzi wa kijamii kwa ajili ya mtoto aliyetajwa hapo juu na kwamba NAPENDEKEZA/SIPENDEKEZI (Futa isiyotakiwa) Malezi ya kambo kama ilivyoelezwa hapo juu.

Saini:

Jina : Tarehe

Afisa Ustawi wa Jamii

7.2 NINAIDHINISHA/SIIDHINISHI (Futa isiyotakiwa) maombi yaliyowasilishwa na mtu/watu binafsi waliyoorodheshwa hapo juu ili wawekwe kwenye arodha ya walezi wa kambo walioidhinishwa.

Saini Tarehe

Kamishna wa Ustawi wa Jamii

7.3 Uidhinishaji mbadala wa Afisa Ustawi wa Jamii (kama iliyoanishwa chini ya Kanuni 8(6) ya Kanuni za malezi ya kambo).

Saini:

Jina :

Tarehe

Afisa Ustawi wa Jamii

Kanuni za Malezi ya Kambo

SHERIA YA MTOTO

KANUNI ZA MALEZI YA KAMBO 2011
(TANGAZO LA SERIKALI NA. ...LA 2011)

F.C Fomu Na. 8

TAARIFA YA KITABIBU

Kanuni ya 15(8)

(Ijazwe na Daktari)

Jina la Daktari anayefanya vipimo
Jina la kituo cha afya
Tarehe ya kufanya vipimo vya mtoto

1. Taarifa za msingi

Jina la mtoto
Jinsi (me/ke)
Tarehe ya kuzaliwa
Urefu Uzito

2. Kumbukumbu za chanjo

	Chanjo	Tarehe		Chanjo	Tarehe
Polio			Donda koo		
Ndui			Pepopunda		
BCG			Kifaduro		
Nyingine			Mengine		

3. Historia binafsi

Je aliyepimwa ugua kuugua yafuatayo?

Kama ndiyo onyesha dhidi ya vipimo, ikiwa siyo, tafadhali andika “HAPANA” katika sehemu husika

1. Kifua kikuu
2. Vidonda vya tumbo
3. Kuvimbiwa
4. Kuhara
5. Homa ya manjano
6. Kisukari
7. Polio au ugonjwa wa uti wa mgongo

8. Kifafa
9. Kuchanganyikiwa kiakili
10. Maradhi ya akili
11. Matatizo ya macho
12. Matatizo ya sikio, pua na koo
13. Magonjwa ya ngozi
14. Upungufu wa damu mwili
15. Matatizo ya uzazi
16. Malaria au magonjwa mengine ya kitropiki
17. Kipindupindu
18. Upasuaji
19. Ajali mbaya

Kama umejibu ndiyo kati ya yaliyotajwa juu, toa maelezo ya ziada:

.....
.....

4. Uchunguzi wa kitabibu

4.1 Afya kwa ujumla

Afya kwa ujumla

Hali ya ngozi.....

Meno koo

Kupanuka kwa tezi

Macho (mboni)

Mfumo wa hewa

Mfumo wa mishipa ya damu ya moyo

Tumbo

Hali mbaya

Mfumo wa neva

Hali ya VVU

4.2 Uchunguzi

1. Upimaji mkojo wa mara kwa mara

2. Choo

3. Hb %

4.3 Matokeo

Je mtoto hana magonjwa ya kuambukiza?

Tatizo lolote kubwa la ulemavu:

Matokeo ya uchunguzi wa Daktari:

Mapendekezo ya Daktari

.....

.....

.....

Saini ya Daktari na tarehe

.....

Dar es Salaam,
27 Machi, 2012

HADJI H. MPONDA,
Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii